

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

AnwaniyaSimu:”UCHUNGUZ  
SimuNambari: 028-2762630  
Nukushi: 028 - 2763358  
Baruapepe:pccbshinyanga.go.t



MKUU WA TAKUKURU MKOA  
Mtaa wa Uzunguni,  
S.L.P 37,  
37101 SHINYANGA,  
Tanzania.  
Simu: (028) 2762630  
Nukushi: (028) 2763358

---

09, Oktoba 2019.

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### **LEO TAREHE 09, OKTOBA, 2019 TAKUKURU SHINYANGA INATARAJIA KUMFIKISHA MAHAKAMANI HAKIMU MKAZI WA MAHAKAMA YA MWANZO KISHAPU NDG. BENJAMIN CHARLES MHANGWA KWA KOSA LA KUOMBA NA KUPOKEA RUSHWA.**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Kishapu, mkoa wa Shinyanga leo tarehe 09, Oktoba, 2019 itamfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Shinyanga Ndg. BENJAMIN CHARLES MHANGWA ambaye ni Hakimu Mkazi Mahakama ya Mwanzo Kishapu kwa kosa la kuomba na kupokea Rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

Kati ya tarehe 23/09/2019 na 25/09/2019 Ndg. BENJAMIN CHARLES MHANGWA ambaye ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Kishapu alishawishi kiasi cha Sh. 300,000/= kutoka kwa mzazi aitwaye JUMA KATSON MBUGI kwa kumwambia kuwa ametumwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kishapu aitwaye Wilberforce Luwago ili aweze kumsaidia kupata ushindi katika kesi ya kubakwa mtoto wake wa kike iliyokuwa ikisikilizwa katika mahakama hiyo ya wilaya ya Kishapu. Hivyo siku ya tarehe 27/09/2019 ndani ya maeneo ya Kata ya Kishapu Mtuhumiwa alijipatia kiasi cha Sh. 200,000/= kutoka kwa JUMA KATSON MBUGI kupitia VICENT BAHATI MAKOLO ikiwa ni sehemu ya shilingi laki tatu (300,000/=) alizoomba.

Uchunguzi uliofanyika umebaini kuwa fedha hizo hazikuombwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Kishapu WILBERFORCE LUWAGO. Hivyo Mtuhumiwa huyo BENJAMIN CHARLES MHANGWA ambaye ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Kishapu aliomba na kujipatia fedha hizo kwa njia ya udanganyifu.

#### **WITO.**

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga anaendelea kutoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Shinyanga kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU katika kuwafichua wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa, ili kuweza kuwachukulia Hatua za Kisheria.

---

**Imetolewa na H. M. Mussa Kaimu Mkuu wa TAKUKURU (M) Shinyanga.**